



MANABII na MITUME wetu

Yesu Kristo anaongoza Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho kupitia manabii na mitume. Soma kuhusu wao hapa chini. Kisha **kata na uondoe picha kwenye ukurasa wa R23** na uzigandishe mahali pake katika chati. Weka gundi juu ya kila picha ili uweze kuziina kwa ajili ya kusoma kweli zilizoko chini!

- Alisafisha duka la ufundi redio kama kazi yake ya kwanza
- Alikuwa mwanasheria na hakimu wa Juu wa Mahakama ya Utah
- Alikuwa rais wa Chuo Kikuu cha Brigham Young



Rais Dallin H. Oaks

Mshauri wa Kwanza katika Urais wa Kwanza

- Alikuwa daktari mpsuaji wa moyo
- Alijifunza lugha nyingi, ikiwemo Kichina
- Ana watoto kumi: 9 mabinti na 1 wa kiume



Rais Russell M. Nelson

Rais wa 17 wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho

- Alicheza mpira wa kikapu akiwa shule ya upili
- Alijifunza fizikia kutoka kwa baba yake kwenye ubao wa chaki wa familia yao
- Alikuwa rais wa Chuo cha Ricks, sasa Chuo Kikuu cha Brigham Young-Idaho



Rais Henry B. Eyring

Mshauri wa Pili katika Urais wa Kwanza

- Alipewa jina la utani la "askofu" alipokuwa chuoni kwa sababu ya viwango vyake vya juu
- Alikuwa mfanyabiashara wa magari
- Alitumikia kama mmisionari huko Uingereza na kama rais wa misheni huko Toronto, Kanada



Rais M. Russell Ballard

Kaimu Rais wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

- Alikuwa mwenza mmisionari wa Mzee Cook huko Uingereza
- Alifanya kazi kwenye Mfumo wa Elimu wa Kanisa
- Alikuwa rais wa Chuo Kikuu cha Brigham Young



Mzee Jeffrey R. Holland

Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

- Alikuwa mkiimbizi mara mbili alipokuwa mtoto
- Alikuwa rubani wa ndege
- Hufurahia kuteleza kwenye theluji na watoto wake pamoja na wajukuu



Mzee Dieter F. Uchtdorf

Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

- Alikuwa mlinzi kwenye timu yake ya mpira ya shule ya upili
- Baada ya kutumikia misheni huko Ujerumani, alimbatiza baba yake kuwa muumini wa Kanisa
- Alikuwa rais wa Chuo cha Ricks wakati kilipokuwa Chuo Kikuu cha Brigham Young-Idaho



Mzee David A. Bednar

Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

- Alipata ushuhuda baada ya kusoma maandiko na kuomba pamoja na kaka yake mkubwa
- Alimwona mkewe mtarajiwa kwenye onyesho la vipaji katika shule ya upili.
- Alitumikia kama kiongozi wa Kanisa huko Ufilipino na Visiwa vya Pasifiki



Mzee Quentin L. Cook

Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

- Alioka mkate wa nyumbani kwa ajili ya familia yake changa
- Alishiriki katika tamasha la Mlima Cumorah huko New York akiwa kijana aliyebalehe
- Alifanya kazi kama mwana-sheria kabla ya kuitwa kama Mtume



Mzee D. Todd Christofferson

Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

- Alikulia katika shamba la kufugia ng'ombe huko Idaho, Marekani
- Alitumikia kama mmisionari na rais wa misheni huko Ufaransa
- Anazungumza Kifaransa, Kireno, Kihispania, na Kiingereza



Mzee Neil L. Andersen

Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

- Alikuwa rais wa misheni huko New York, Marekani
- Kauli mbiu yake ni "Ni watu ndio wenye umuhimu mkubwa"
- Aliweka wakfu jengo la kwanza la Watakatifu wa Siku za Mwisho huko Jamhuri ya Cheki



Mzee Ronald A. Rasband

Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

- Alitumikia kama mmisionari na baadaye kama rais wa misheni ya Japani
- Alianzisha biashara ya kutengeneza na kuuza vifaa vya mazoezi
- Alitumikia kama askofu wa Kanisa lote



Mzee Gary E. Stevenson

Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

- Jina lake la katikati, Gunnar, linamaanisha "askari shujaa"
- Alihama na familia yake kutoka Utah kwenda Sweden alipokuwa na miaka 11
- Alifanya kazi kama daktari wa moyo



Mzee Dale G. Renlund

Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

- Anapenda wanyama, ikijumuisha pengwini
- Hupenda kukutana na watu katika kila nchi
- Ana rekodi ya historia ya familia inayorudi nyuma mpaka kwa Dragon Gong wa kwanza miaka 837 Baada ya Kristo.



Mzee Gerrit W. Gong

Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

- Anatokea Brazil na alitumikia kama mmisionari huko na kama rais wa misheni ya Urusi
- Alijifunza kuhusu Kanisa pamoja na familia yake kama mvulana mdogo
- Alianza kujiandaa kwa umisionari alipokuwa na miaka 12



Mzee Ulisses Soares

Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

Angalia jibu lako kwenye [lds.org/prophets-and-apostles](https://www.lds.org/prophets-and-apostles).